


| Neno | Maelezo | Picha |
|--|---|---|
| Kukata kiungo | Kupoteza sehemu ya mwili, kwa mfano mguu au mkono | |
| Maumivu kwemye maungio ya viungo viwili | Tatizo la kiafya, ambapo sehemu za maungio ya mtu zinakuwa ngumu na kuvimba na/ au kuwa na maumivu wakati mtu anapojaribu kuziinua. | |
| Mfupa uliovunjika (frakcha) | Kuvunjika kwa mfupa. | |
| Ugonjwa wa kisukari | Ugonjwa ambao unaambatana na mtu kuwa na sukari nyingi kwenye damu. Hii inaweza kusababisha matatizo ya kiafya ikiwemo; kutokuwa na hisia kwenye sehemu za mwili (kwa mfano kwenye miguu) na vidonda kwenye shemu za kukanyagia za mtu, kupoteza uwezo wa kuona, kuharibika kwa figo, kupata ugumu kwenye kudhibiti mkojo na kukumbuka vitu kwa taabu. | |
| Kidonda sehemu ya kukanyagia ya mguu | Ngozi ya sehemu ya kukanyagia ya mguu kukatika katika. Vidonda vya mguu vinatokana na madhara yatokanayo na ugonjwa wa kisukari. Kama vidonda vya kwenye sehemu ya kutembelea ya mguu havijatibiwa; inaweza kupelekea mguu kukatwa. Aidha, vindonda vya kwenye sehemu ya mguu vinaitwa michubuko ya sehemu ya kutembelea ya mguu |  |
| Udhaifu | Hii ni kutokuwa na nguvu, kuumia kwa urahisi au kuwa na nguvu kidogo. Hutokea pale mtu anapokuwa kiumri na afya inapoanza kudorora. | |
| Mkono kufanya kazi | Uwezo wa mkono kufanya kazi, kwa mfano kuandika, kubeba vitu, kuandaa chakula na kushona. | |
| Kupooza | Kutokuwa na uwezo wa kusogeza sehemu ya mwili (mara nyingi miguu au mikono). | |
| Polio | Ni ugonjwa mbaya ambao unasababisha misuli ya mgonjwa inakosa nguvu au inapooza. Hii inaathiri uwezo wa kutoka eneo moja hadi jingine hata baada ya kupona maradhi. | |

| | | |
|--|---|---|
| <p>Mguu bandia au sehemu ya kutembelea ya mguu ambayo ni bandia</p> | <p>Ni mguu bandia au sehemu ya kutembelea ya mguu ambayo inachukua sehemu ya mguu na sehemu ya halisi ya kutembelea kwa binadamu.</p> |  |
| <p>Kiharusi</p> | <p>Damu kutokuweza kufika kwenye ubongo. Hii inaweza kusababisha sehemu ya mwili kukosa nguvu au kupooza pamoja na kuongea kwa taabu, kuhisi kwa taabu, kufikiria kwa taabu na kuona kwa taabu.</p> | |
| <p>Viatu vizuri kutembelea</p> | <p>Viatu vinapatikana kwenye maeneo ambayo mtu anaishi, vinamkaa vizuri mvaaji na vina vitu vya kuweza kuulinda mguu na kupunguza uwezekano mtu kuanguka.</p> |  |
| <p>Viatu tiba</p> | <p>Viatu ambavyo vina vitu vinavyosaidia kulinda mguu na kusaidia sehemu ya kutembelea ya mguu ambao uko katika hatari ya kupata kidonda.</p> |  |
| <p>Uwezo wa kubeba mwili</p> | <p>Kiwango cha uzito ambacho mtu anaweza kubeba kwa m(i)guu yake.</p> | |